# Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi

**F.E.M.K. Senkoro**

## Ikisiri

Makala hii inatalii maana ya fasihi ya Kiswahili ya majaribio, kwa kupitia kanuni za kifasihi simulizi ambazo zinaelekea kuwa msingi na mwimo wa majaribio hayo. Makala inaonyesha kuwa kanuni hizi ndizo ambazo zimejidhihirisha hata katika fasihi ya Kiswahili ya hivi karibuni ya waandishi waliofanya majaribio ya aina mbalimbali, wakiwemo wa tamthilia, riwaya na hadithi fupi. Makala inatumia zaidi mifano kutoka katika tamthilia za *Lina Ubani* (P. Muhando) na *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* (E. Hussein) na pia riwaya ya *Rosa Mistika* (E.Kezilahabi) kueleleza majaribio hayo. Swali ambalo hatimaye linajadiliwa ni, je, majaribio haya yanafuata kanuni zipi? Upya una nafasi gani katika majaribio? Na, je, majaribio mahsusi ya fasihi fulani yanaanza na kuisha wakati gani?

## 1.0 Utangulizi

Kanuni za utanzu wowote wa fasihi huambatana na kuamuliwa na maana ya utanzu huo. Tuongeapo kuhusu kanuni za uwanja fulani wa fasihi hapohapo tunajaribu kuangalia yale mambo yajitokezayo mara kwa mara katika uwanja huo. Pia tunazingatia ukweli kuwa kanuni hizo hazibakii hivyohivyo kwani huweza kubadilika kufuatia mabadiliko katika utanzu unaohusika.

Kwa vile majaribio mengi yaliyofanyika katika fasihi andishi ya Kiswahili yanaelekea kuwa yamechota kutoka katika fasihi simulizi ya Kiswahili / Kiafrika, makala inaanza kwa kuzipitia kanuni hizo za fasihi simulizi - kanuni mahsusi zinazoifanya fasihi simulizi ijitegemee. Kanuni hizi huzoeleka tangu wanajamii wengi wakiwa watoto wadogo wanapotambiwa na wakubwa wao hadithi, visa, na ngano; wanapotegewa vitendawili pamoja na mafumbo, na kadhalika. Katika makala hii tumechagua kanuni 12 tu kati ya kanuni nyingi, nazo ni:

- Uelezwaji au utambwaji
- Sifa anazopaswa kuwa nazo mtambaji
- Hadhira na nafasi yake katika uelezaji/utambaji
- Taswira na Ishara
- Mianzo na Miisho ya Kifomula
- Marudiorudio
- Taharuki

- Ucheshi
- Tanakali sauti
- Kuingiliana kwa tanzu
- Muundo
- Majina ya wahusika

## 2.0 Nafasi ya Utambaji na Mtambaji

### 2.1 Utambaji

Fasihi haiwi fasihi simulizi hadi itambwe na itolewe kwa njia ya mdomo. Uelezaji au utambaji mara nyingi hutegemea aina ya hadhira. Kwa mfano, utambaji katika utanzu uleule mmoja, tuseme wa misemo, utaweza kutofautiana kulingana na hadhira: misemo itakayotolewa kwa watoto wadogo ni dhahiri kuwa itatofautiana na ya watu wazima. Uelezaji na utambaji wa tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kwa watoto wakati huohuo hutumika kuwapa mazoezi ya usemaji na utambaji ili wawapo watu wazima nao wawe wasanii; na pia wawe watumiaji wazuri wa lugha katika maongezi, hotuba na kadhalika. Wakati huohuo, utambaji huwafundisha watoto kuwa na kumbukumbu za mambo wanayoelezwa na pia wanayoyaeleza.

Uelezaji huu hauwezi kukamilika bila kuwa na mtambaji mzuri kwani, ijapokuwa katika fasihi simulizi kila mtu ana uhuru wa kueleza kisa, hadithi au ngano aliyokwishaisikia kwa mwingine, si kila mtu anaweza kuwa mtambaji bora. Katika fasihi simulizi za jadi hapakuwa na sheria za "haki za kunakili" kama zilizopo leo katika baadhi ya tanzu za fasihi hii, kwa mfano katika nyimbo za bendi zilizorekodiwa.

Mtambaji anatakiwa awe na sifa kadhaa. Kwanza, awe na uwezo wa kuipa upya habari yoyote anayoieleza ili kuifanya hadhira iifurahie kwani aghalabu hutokea kuwa baadhi ya wanahadhira wameshawahi kuisikia habari hiyo ikitambwa na mtu mwingine. Ufundi wa utambaji hujitokeza hasa katika kuielewesha hadhira ufafanuzi wa yale mtambaji ayaonayo hayajaeleweka vizuri lakini wakati huohuo *aweze kuitoa habari hiyo kiupya na kisanii bila kuhubiri.* Mtambaji basi huwa ni msanii, mburudishaji, mwelimishaji na mtoa maoni kuhusu masuala ya kijamii yanayoigusa hadhira yake.

Pili, ili aweze kuyamudu yote hayo, msanii hana budi awe anaufahamu fika utamaduni na historia ya jamii ambamo yale ayaelezayo yametoka. Hana budi kutopea katika mila na jadi anazoziibusha katika maudhui ya habari anayoishughulikia. Inamlazimu awe mtaalamu wa lugha aitumiayo na awe mjuzi wa misemo, nahau, taswira na ishara mbalimbali zinazojenga jambo analolieleza.

Iwapo mtambaji anawapa vijana mazoezi ya kukumbuka mambo wanayoelezwa, inabidi yeye mwenyewe awe na sifa hii ya kumbukumbu. Hana budi kuwa mtu mwenye uwezo wa kutunga na pia kuing'amua hadhira yake pale inapombidi, kwa

mfano, abadili mtindo wake labda kwa kuinghiza wimbo hata pale ambapo utanzu anaoushughulikia si ule wa nyimbo..

Mtambaji huyu huyu hatakiwi awe na aibu bali awe mtu mchangamfu mwenye kuifurahia habari anayoieleza ili pale anapohitajika kutia madoido afanye hivyo, na pale inapombidi kutumia maneno ambayo katika muktadha mwingine yangekuwa matusi, asione aibu kuyatumia kifasihi simulizi. Wakati huohuo mtambaji ni mwigizaji kwani aghalabu anahitajiwa achukue nafasi za wahusika mbalimbali, wanawake kwa wanaume, watoto kwa wakubwa, wanyama kwa binadamu.

Mtambaji hatakiwi awe anafahamu historia, mila, utamaduni na jadi za kale tu. Anatakiwa pia afahamu fika nguvu mbalimbali za kijamii za leo; na awe daraja kati ya nguvu hizo na zile za mambo ya kale, kwani *fasihi simulizi si juu ya mambo ya zamani tu bali pia huhusu yale yatokeayo leo.*

## 2.2 Nafasi ya Hadhira katika Utambaji

Hadhira, sawa na mtambaji, ni muhimu sana katika uelezwaji na upokelewaji wa fasihi simulizi. Hadhira ni kichocheo kinachoimarisha uelezwaji na utambwaji wa fasihi hii. Huongezea ari ya ubunifu wa mtambaji, na wakati mwingine huweza hata kumsahihisha au kumsaili mtambaji.

Mara kwa mara hadhira pia huwa sehemu ya utambaji kwa kushiriki katika sehemu mbalimbali, kwa mfano, penye kiitikio, mkarara na matumizi ya nyimbo, kutegua vitendawili, kumalizia methali, na hata kupiga makofi.

Hata hivyo kiasi cha kushiriki kwa hadhira hutegemea jambo linaloelezwa. Iwapo jambo lielezwalo ni zito lenye kuhitaji tafakuri na kuwaza kwa undani, hadhira mara nyingi hubaki kimya bila kushiriki ila tu pale panapohitaji maswali yaulizwe au majadiliano yafanywe; ijapokuwa mara nyingi hili hutokea mwishoni baada ya habari kuelezwa.

Kwa hiyo basi, tunaweza kusema kwa jumla kuwa uhakiki wa fasihi simulizi ni wa papo kwa papo kwani katika kushirikiana na fanani au msanii hadhira huihakiki pia kazi itolewayo. Kwa kuihakiki hivi, msanii au mtambaji hurekebisha maelekezo yake au huyaelekeza kule hadhira inapotaka.

## 2.3 Mtambaji na hadhira katika fasihi ya Kiswahili ya majaribio

Katika fasihi ya Kiswahili ya majaribio, hasa katika tamthilia, waandishi wamezichota sifa za mtambaji na kuzihamishia katika mtiririko wa tamthilia zao. Mathalani, Bibi na Mwenehogo katika tamthilia ya Penina Muhando ya *Lina Ubani* na mhusika mwenye jina hasa la Mtambaji katika tamthilia za E. Hussein ya *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* wametumiwa sana na waandishi hawa kuwa kiungo baina ya hadhira na wahusika wengine pamoja na matukio muhimu ya tamthilia hizi. Tangu mwanzo

wa tamthilia, wahusika hawa wanaowawakilisha watambaji wa hadithi wanazianza tamthilia kwa fomula ya kihadithi, na kila mara wametumiwa na wanatamthilia hawa kufafanua yanayotokea katika mfululizo wa visa mbalimbali.

Watambaji katika tamthilia hizi wanakuwa kama waelezaji wa hadithi ndani ya hadithi, wanaunda hadithi mbadala ambazo hata hivyo zinazijenga "hadithi" za msingi za tamthilia hizi. Wahusika hawa wanakuwa kama vile wanaishirikisha hadhira katika kuiunda tamthilia. Ndio maana, kwa mfano, Mwenehogo katika *Lina Ubani*, ijapokuwa ni mchekeshaji, tena mlevi, anatumiwa mara kwa mara kuunda "vihadithi" vya kuichekesha hadhira, lakini vyenye kubeba ujumbe mzito unaohusiana na dhamira anazozishughulikia Penina Muhando. Vivyo hivyo, Mtambaji katika *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* anapomwongelea kijana anayepigana na joka anamwita "kijana wetu" ili kifanya hadhira ijisikie kuwa hadithi au kisa kinachoelezwa si cha mtambaji tu bali ni cha wote wanaoitazama au kuisoma tamthilia. Katika kuzitamba hadithi zao, wahusika hawa wana jukumu la kuitahadharisha hadhiya ya watazamaji au wasomaji kuwa yanayoelezwa si ukweli au uhalisi bali ni mwigo tu wa ukweli na uhalisi huo.

Katika kujaribu kuishirikisha hadhira kwenye tamthilia hizi, watambaji wanauliza maswali hapa na pale, hasa kwa njia ya kiitikio, ili kujaribu kukaribia hali halisi ilivyo ya ushirikishwaji wa hadhira katika fasihi simulizi. Mathalani, mhusika Mtambaji katika *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* daima hujaribu kuwaamsha watazamaji/ wasomaji kwa kuwauliza kama aendelee au asiendelee na kisa anachokieleza, na hadhira inatakiwa kujibu, "Endelea!" sawa na vile ambavyo watoto walizoea kumjibu bibi au babu wakati akitamba hadithi.

Ni katika tamthilia hizi hizi ndimo ambamo watambaji wanamalizia utambaji wao kwa kuomba wapewe mji. Tamthilia zinamalizika kwa fomula ya vitendawili, na kwa hakika, wahusika hawa wanapotuomba mji sisi hadhira, na tunapowapa miji hiyo, wanaahidi kututegulia vitendawili vilivyofumbwa katika tamthilia hizi. Ila, kinyume na ilivyo katika fasihi simulizi, humu hatupewi jibu. Ni kama kwamba tunatakiwa turudi nyuma, tuzisome au kuziangalia upya tamthilia hizi ili kupata majibu yatakayotutegulia *utendawili* uliomo ndani yake. Tendo la kuzisoma upya na kuyatafakari kwa undani zaidi yale yaliyosimuliwa katika tamthilia hizi ndilo uteguaji wa kitendawili.

Hata hivyo, nionavyo mimi, mwishoni mwa *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* hadhira inabaki na maswali zaidi ya mwishoni mwa *Lina Ubani*. Utendawili wa *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* unadhihirika zaidi kwani visa vimefumbwa mno kiasi cha kujiuliza mwandishi alimaanisha nini; kuliko ule wa *Lina Ubani* ambao umepatiwa majibu yasiyohitaji maswali. E. Hussein, basi, ana haki na stahili ya kuitaka hadhira impe mji kuliko P. Muhando.

## 3.0 Fani katika Fasihi Simulizi

Ni vigumu kutoa kauli ya jumla kuhusu fani katika fasihi simulizi, kwani hii itategemea utanzu unaohusika pamoja na maudhui yanayotolewa katika utanzu huo. Hapa tutaeleza kwa kifupi tu baadhi ya vipengele *vinavyoweza* kujidhihirisha katika fani ya fasihi simulizi kwa jumla.

### 3.1 Taswira na Ishara

Mara kwa mara utolewaji wa fasihi simulizi hutegemea sana matumizi ya taswira na ishara, hasa katika tanzu za ngano-tata, methali, vitendawili na habari za kimafumbomafumbo. Hapa yamejaa matumizi ya tamathali za semi zenye kufananisha watu na vitu, au vitu vya aina moja na vya aina nyingine, na kadhalika. *Uhuru wa kisanii* humruhusu mtambaji, kwa mfano, katika kuelezea ujasiri wa shujaa mmoja, aseme kwa dhati kuwa moyo wa shujaa huu haukuwa wa kawaida, ulitengenezwa kwa mawe. Moyo wa jiwe hapa ni ishara ya ugumu wa moyo huo wenye kutoa taswira ya ushujaa na ujasiri.

Waandishi wa tamthilia za *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* na *Lina Ubani* wametumia ishara kadhaa pia katika visa vya kazi zao. Mathalani, Zimwi ambalo linajitokeza katika *Lina Ubani* na Joka katika *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* huweza kuwa ishara ya mfumo wa kiutawala wa mabavu, wakati ambapo Huila na Kijana katika tamthilia hizi ni viwakilisho vya wapigania uhuru na watetea haki katika jamii zao. Vilevile, ndani ya hadithi ya Iddi Amin Dada ambayo inajitokeza katika *Lina Ubani* mna kiwakilisho cha zimwi hilo - kiwakilisho cha utawala wa aina hiyo. Taswira na ishara nyingine ambazo tunaweza kujiuliza zinawakilisha nini ni, kwa mfano, mkunazi rahmani na jogoo katika *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi.*

### 3.2 Mianzo na Miisho ya Kifomula

Katika jamii mbalimbali kuna mianzo ainaaina ya utoaji wa tanzu tofautitofauti za fasihi simulizi. Hapa tutatoa mifano michache to ijitokezajo katika fasihi simulizi ya Kiswahili.

Upande wa vitendawili mtoa kitendawili huanza na:

Mtambaji: Kitendawili!
Hadhira: Tega

Baada ya mwanzo huu wa kifomula ndipo kitendawili kinapoteguliwa. Iwapo hadhira itashindwa kukitegua basi mtegaji huomba "mji". Akubalipo mji aliopewa hapo huitegulia hadhira kitendawili hicho. Hii tabia au mtindo wa kuomba "mji" ni dhahiri kabisa kuwa ulitokea katika jamii za baadaye sana baada ya kuzuka kwa miji. Katika makabila mbalimbali mtegaji aliomba apewe ng'ombe au mali yoyote iliyotokana na mazingira yaliyohusika.

Upande wa utanzu wa ngano au visa, na hadithi, mianzo iko ya aina nyingi zaidi, labda kwa sababu utanzu huu umesambaa zaidi ya nyingine za fasihi simulizi.

Mwanzo au kianzio kilichoenea ni cha fomula ya:

Mtambaji: "Hadithi hadithi"
Hadhira: "Hadithi njoo"
Mtambaji: "Hapo zamani za kale..."

Mwingine ni:

Mtambaji: "Paukwa"
Hadhira: "Pakawa"
Mtambaji: "Paukwa"
Hadhira: "Pakawa"
Mtambaji: "Hapo kale alikuwako..."

Wakati mwingine baada ya hizo "paukwa-pakawa" mtambaji huweza kurefusha kianzio kwa:

Mtambaji: "Kaondokea chenjagaa
Kajenga nyumba kakaa
Mwanangu Mwana siti
Kijino kama kijiti
Cha kujengea kikuta
Na vilango vya kupita.
Hapo kale alikuwako..."

Pia hutokea kuwa kabla ya kianzio hiki, badala ya "paukwa- pakawa" mtambaji huanza kama ifuatavyo:

Mtambaji: "Atokeani"
Hadhira: "Naam Twaibu"
Mtambaji: "Atokeani"
Hadhira: "Naam Twaibu"
Mtambaji: "Kaondokea chenjagaa..."

Kianzio ambacho kimezoweleka sana siku hizi, hasa baina ya watoto ni:

Mtambaji: "Hadithi hadithi"
Hadhira: "Hadithi njoo, uongo njoo, utamu kolea!"
Mtambaji: "Hapo zamani za kale"
Hadhira: "Ehe!"
Mtambaji: "Alikuwako / Walikuwako..."

Kauli hii ya "uongo njoo" haipunguzi uzito wa lile linaloelezwa bali husisitiza tu kuwa jambo hilo linaelezwa kiubunifu na kuwa siyo uhalisi wenyewe.
Kuhusu kumalizia, mara nyingi mtambaji humalizia kwa, "Na hadithi yangu imeishia hapo." Pia mtambaji, hasa baina ya watoto, huweza kumalizia kwa "Hadithi yangu ndiyo hiyo, kama nzuri ipokeeni, kama ni mbaya, nirudishieni."

Katika *Lina Ubani* na *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* fomula hizo za mianzo na miisho zimetumiwa na waandishi pale ambapo tamthilia zimeanza kama hadithi na zimeisha kama vitendawili.

### 3.3 Marudiorudio

Katika fasihi simulizi, kuna nia tofautitofauti katika matumizi ya mbinu ya kurudiarudia kauli au neno fulani yanayofanywa na watambaji.. Wakati mwingine si kauli au maneno tu yanayorudiwa bali pia matukio fulani, wazo fulani, au mkarara/ kiitikio, hasa katika nyimbo.

Marudio marudio hayo yanatumiwa na wasanii kwa makusudi tofautitofauti. Wakati mwingine hutumiwa ili kusisitiza jambo fulani la kimaudhui analotaka kulionyesha fanani au msanii. Mara nyingine marudio marudio haya yanasaidia kutoa dhana ya kupita kwa wakati. Kwa mfano, iwapo mtambaji anataka kueleza juu ya muda mrefu sana uliopita baina ya tukio moja anaweza kusema:

Siku zikapita
Siku zikapita
Siku zikapita
Zikageuka kuwa miezi

Miezi nayo ikapita
Ikapita
Ikawa miaka ambayo pia
Ilipita
Ikapita
Ikapita

Vuli zikaja zikapita
Masika yakawasili yakapita

Vipupwe na viangazi vikaja na kupita
Lakini bado
Bwana yule na mkewe
Hawakupata mtoto
Na ugumba na utasa ukaendelea..."

Hapa ni dhahiri kwamba marudio yanatufanya sisi hadhira tuipate dhana ya wakati vizuri zaidi kuliko kama mtambaji angesema tu "siku nyingi zikapita ila yule bwana na mkewe hawakupata mtoto."

Maridiorudio yametumiwa na waandishi wa tamthilia za Kiswahili za majaribio kwa lengo hilo hilo la kuponyesha kupita kwa wakati. Mathalani, katika tamthilia ya *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* dhana hii ya wakati imeelezwa katika schemu mbalimbali kwa kurudiwa kwa kauli ya:

Miaka ikapita,

miaka ikapita,
miaka ikapita;
watu wakaoana,
watu wakazaana
na kaumu ikazidi.

Inakuwa ni jukumu la hadhira kukadiria wingi wa miaka hiyo iliyopita, na hasa kutokana na kitendo cha watu kuzaana na kaumu kuongezeka.

### 3.4 Taharuki

Sawa na katika fasihi andishi, tanzu mbalimbali za fasihi simulizi hutumia mbinu ya taharuki ili kuvuta usikivu wa hadhira. Hii hufanya hadhira kujiuliza mara kwa mara kuhusu matukio yatakayofuatia kuwa yatakuwa ya namna gani.

Ujengaji wa taharuki hutofautiana kutoka mtambaji mmoja hadi mwingine, hata kama kisa kinachoelezwa ni kilekile kimoja. Mtambaji mwenye ujuzi, uzoefu na kipawa zaidi atafaulu kuishikilia hadhira yake katika uzi wa taharuki zaidi ya yule ambaye ndio kwanza anauingia ulimwengu wa utambaji.Ufundi wa kuishikilia hadhira katika taharuki unaweza kuletwa si kwa yale yanayoelezwa tu bali pia **jinsi** yanavyotolewa na mtambaji. Mabadiliko ya sura ya mtambaji, kwa mfano, huweza kuifanya hadhira ijue kuwa jambo litakaloelezwa baada ya muda mfupi ni la kutisha, kwa hiyo wawe na taharuki na ari ya kulisubiri. Hata mabadiliko ya kiimbo cha sauti ya mtambaji huweza pia kuleta hali hiyo ya taharuki.

Mbinu nyingine itumiwayo pia katika fasihi andishi ili kuumba hali ya taharuki ni ile ya kuchelewesha matukio fulani au majibu ya maswali fulani ambayo msimuliaji huyafanya yawazukie wasikilizaji au watazamaji wake. Haya hucheleweshwa hadi baadaye sana wakati ambapo hadhira huwa imekwishaning'inizwa katika kamba ya taharuki kwa muda mrefu.

Kwa mtambaji mahiri majibu yote hutolewa, au yale ambayo hayatolewi yanaachwa kwa makusudi kabisa ili hadhira irudi nyuma na kutafakuri yaliyotambwa.

Waandishi wa tamthilia ya Kiswahili ya majaribio nao hali kadhalika wameitumia mbinu hii ya taharuki. Kwa mfano, kisa anachokieleza Mtambaji katika *Ngao ya Jadi*, kinatufanya sisi tuambatane na Kijana katika mapambano na Joka lenye vichwa sabini huku tukiwa na shauku ya kujua hatima ya mapambano haya. Katika nyoyo zetu, tunataka Kijana ashinde kwenye mapambano haya, lakini tunashikwa na shauku kwani tunajua kuwa anapambana na adui ambaye si wa kawaida; anapambana na joka la vichwa sabini. Je, ataweza kuvidengua vichwa hivi, kimoja hadi kingine?

### 3.5 Ucheshi

Mbinu ya ucheshi, sawa na nyinginezo za fani, hutumiwa na mtambaji kwa nia tofautitofauti. Kama ilivyo katika baadhi ya kazi za fasihi andishi, vivyo hivyo

katika fasihi simulizi ucheshi hutumiwa kuwa kipumuo, hasa baada ya matukio ya kutisha au maelezo marefumarefu yenye kuwachosha wasikilizaji. Mbinu hii huweza kutumiwa, kwa mfano, pale ambapo mtambaji labda kaiweka hadhira yake katika hali ya taharuki kwa muda mrefu, au kaieleza juu ya mambo ya kitanzia na ya kusikitisha, na sasa wanahitaji kupumua na kutabasamu kidogo.

Katika *Lina Ubani* maneno ya mhusika Mwenchogo yana ucheshi mwingi sana ndani yake, ucheshi ambao unatufanya sisi watazamaji au wasomaji tuburudike na kupumua wakati tukitafakari mivutano iliyopo baina ya akina Huila na wanasiasa. Hata *Ngonjera* ya Mota inatufanya tutabasamu tunapoona namna mtoto anavyoitafsiri hadithi ya kiutu uzima inayoelezwa na Bibi.

## 3.6 Tanakali sauti

Maneno ya ki-tanakali sauti ni yale ambayo yanaigiza sauti ya kitu fulani au tendo fulani. Haya yameenea sana katika tanzu mbalimbali za fasihi simulizi, nayo yanasaidia sana kuyafanya yale anayoyaeleza mtambaji yaeleweke kwa hadhira yake. Yanasaidia sana kukamilisha hisia za hadhira, kwani mara nyingi hushughulikia milango yote mitano ya fahamu za mtu: ya kunusa, kusikia, kuona, kuhisi, na kuonja.

Katika *Jogoo Kijijini*, kwa mfano, E. Hussein katumia mbinu hii mara kadhaa kuumba hali anayotaka iumbike akilini mwa hadhira. Mtambaji kasema, mathalani:

..... Mara
Kupi
Jua lilikupiza
Pa
Mwanga kajikatiza
Zi
Na giza kaingia (uk. 17)

Maneno "kupi", "pa" na "zi" ni ya kitanakali-sauti, ijapokuwa "sauti" zenyewe ni za kuwazika tu kwani hakuna mtu aliyewahi kusikia "sauti" ya jua likikupiza, ya mwanga ukijikatiza, au ya giza likiingia.

## 3.7 Kuingiliana kwa Tanzu

Kutumiwa kwa utanzu mmoja wa fasihi simulizi katika utolewaji wa utanzu mwingine ni mbinu ya kifani itumiwayo na wasanii wa fasihi hii kwa nia mbalimbali. Kwa mfano, si jambo geni kukuta wimbo, au kipande cha wimbo, ndani ya ngano au hadithi. Wimbo, au kipande hiki, huweza kutumiwa ili kuleta msisitizo wa jambo fulani aonalo mtambaji kuwa lina umuhimu, na kwa hiyo katika wimbo huo maudhui ya jambo hilo yanarudiwa. Pia huweza kutumiwa kama njia ya kuondoa uchovu pale ambapo msanii anang'amua kuwa ametoa maelezo marefu mno ya kinathari. Hapa msanii huweza kubadili pia na kuingiza mbinu za ushairi.

Baadhi ya wasanii au watambaji hutumia mbinu za kuingiza tanzu nyingine katika kazi zao kuwa njia ya kuleta mtiririko wautakao utakaounganisha sehemu na sehemu katika visa vyao. Mara nyingi tanzu ndogondogo kama vile methali, vitendawili na misemo hujitokeza sana hasa katika ngano, visa, na hadithi. Hizi hutumiwa na wasanii katika kuimarisha maudhui ya tanzu zao, na aghalabu methali hutumiwa mwishoni mwa utambaji ili hadhira ilipate fundisho humo.

Waandishi wa tamthilia za Kiswahili za majaribio nao hali kadhalika waliitumia mbinu hii ya kuingiliana kwa tanzu katika tamthilia zao. Kama ilivyokwishakuelezwa, pamoja na kwamba vitendawili na ngano ni tanzu mahsusi zinazojitegemea katika fasihi simulizi, waandishi hawa wamezichanganya tanzu hizi na ule wa tamthilia ambao kwa hakika ni utanzu mgeni wakaunda tamthilia mpya. Katika *Lina Ubani* pia, utanzu wa wimbo umejitokeza sana, na tunauona katika wimbo wa Bibi ambao kwa hakika ni sehemu ya hadithi inayotambwa. Hali hii ya kuingiliana kwa tanzu za fasihi simulizi inatia shaka namna ambavyo wanazuoni wamekuwa wakiziainisha tanzu hizo. Inawezekana kabisa kuwa tanzu za fasihi simulizi ya Kiafrika hazitakiwi kuainishwa mojamoja; lakini hili linahitaji utafiti zaidi.

## 3.8 Muundo

Si rahisi kutoa kauli ya dhati kuhusu miundo ya tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kwani tanzu hizi ni nyingi na zinatofautiana kutoka sehemu hadi sehemu.

Muundo rahisi kuueleza ni ule wa vitendawili ambavyo daima huwa na mianzo na miisho ya kifomula. Kwamba miundo hufuatana na mianzo na miisho ya tanzu mbalimbali ni rahisi kuelezeka. Lakini hii ni mianzo na miisho tu. Yaliyomo katikati yake, ambayo aghalabu ndiyo muhimu, yana utata kueleza miundo yake. Tuwezalo kufanya hapa ni kutoa kauli ya jumla tu kuhusu kigezo hiki.

Kuna visa, ngano, na hadithi ambazo miundo yake ni ya moja kwa moja. Muundo hapa unamaanisha mfuatano au mtiririko wa matukio, vitendo, na hata mawazo yalivyopangwa. Kwa hiyo, katika tanzu hizo zenye miundo ya moja kwa moja matukio yake ni ya moja kwa moja yenye mwanzo, kati, na mwisho; sawa na vile ambavyo siku huanza na alfajiri - asubuhi - adhuhuri - mchana - jioni - usiku. Mianzo ya tanzu hizi mara kwa mara hutoa tatizo au mgogoro, na mgogoro huu hutatuliwa au kuchambuliwa katika sehemu ya kati na hatimaye sehemu ya mwisho huonyesha mgogoro ukiwa umetatuliwa. Mara nyingi tunapofuatilia mgogoro ujitokezao katika kisa chenye muundo wa moja kwa moja hapo hapo huwa tunamfuatilia mhusika mkuu na kubadilika pamoja na kukua kwake, kwani aghalabu mgogoro mkuu humzungukia yeye.

Waandishi wa tamthilia ya Kiswahili ya majaribio nao hali kadhalika wametumia miundo changamani kwani matukio mbalimbali yamejengwa kufuatana na utambaji ambao huenda mbele na kurudi nyuma kama watakavyo watambaji wake. Kwa hiyo,

kwa mfano, *Lina Ubani* inaanza na kilio cha Bibi ambaye kampoteza mwanawe, halafu hatua kwa hatua, tunarudishwa nyuma na mwandishi ambaye anatutaka tuyafuatilie matukio tangu mwanzo hadi kufikia hapa kwenye maombolezo ya Bibi ambayo kwa hakika ni mwanzo wa tamthilia na ni mwisho wa hadithi.Wimbo unaojitokeza katika tamthilia ya mwandishi huyuhuyu ya *Nguzo Mama* ni mfano mzuri pia wa kuingiliana kwa tanzu. Wimbo huu unaorudiwarudiwa na akina mama kwenye tamthilia hii unatakiwa usisistize ugumu wa kuisimamisha *nguzo* ambayo inatakiwa iwakilishe ukombozi wa akina mama hao.

## 3.9 Wahusika

Katika fasihi simulizi kuna wahusika wa aina mbalimbali: watu, wanyama, ndege, wadudu, mimea, na hata vitu visivyo na uhai kama vile mawe. Pia wahusika wa kiajabu-ajabu, wa kuwazika tu kama vile mashetani, hutumiwa katika fasihi hii. Wahusika hawa wote huweza kuingiliana pale ambapo mhusika mtu huweza anakutana na hata kuongea na mhusika asiye mtu kama vile jini, shetani, mti, au hata jiwe. Hali kadhalika, katika ulimwengu wa fasihi simulizi si ajabu kukutana na wanyama, miti, au ndege wanaofanya matendo sawa na ya watu. Si ajabu ndege wakichumbiana, wakioana na kufanya sherehe za harusi kama watu tu.

Wahusika wa aina zote hizi hawawezi kuingiliana na kuongea baina yao katika ulimwengu wa fasihi simulizi tu, kwani hata katika majaribio ya kifasihi andishi, mathalani, katika tamthilia hizo mbili, wahusika watu wanapambana na wahusika wa kiajabuajabu ambao katika hali ya kawaida hawajawahi kuonekana, kushikika wala kusikiwa – zimwi na joka la vichwa sabini.

Hadhira inatakiwa iamini kabisa kuwa wahusika wa aina hii wapo kwani wahusika wote hawa kwa njia hii ama ile, wanahitajiwa wawakilishe tabia, mienendo na matendo ya watu halisi. Kwa mfano ujanja wa mhusika maarufu katika baadhi kubwa ya visa na hadithi za fasihi simulizi za Afrika ya Mashariki, Sungura, unahitajiwa uwakilishe ule wa watu watundu; wakati ambapo "uchinichini" wa Mzee Kobe ni kiwakilisho dhahiri cha wale watu ambao kwa kawaida ni wapole ijapokuwa katika upole wao mmejificha ujanja na hekima.

Sawa na fasihi simulizi ya Afrika Mashariki ambamo Sungura ndiye mhusika mjanja sana, fasihi simulizi za sehemu zingine pia huwa na mhusika apendwaye na maarufu kwa ujanja wake. Kwa mfano huko nchini Ghana mhusika huyu ni Buibui, wakati huko Nigeria mhusika-pendwa ni Kobe. Aghalabu wahusika wajanja huwa ni wanyama au wadudu wadogo. Ujanja wao unapowapumbaza wahusika wakubwa-wakubwa kama vile Tembo, Simba, au Kiboko na kutufanya sisi hadhira tuwaone kuwa ni wajinga, husaidia sana katika kuleta ucheshi ndani ya lile linaloelezwa. Si hivyo tu, bali pia wahusika hawa husaidia sana kujenga maudhui ya kazi za fasihi simulizi. Kwa mfano, kila wawapo washindi dhidi ya wahusika wengine wakubwa tunapata funzo kuwa ushindi katika jambo lolote lile hautokani na umbo, wingi au idadi,

bali hutokana na mbinu, ujanja na utundu. Funzo hili huweza kupanuliwa zaidi na kuwapa moyo watu au mataifa manyonge yanayopigania haki zao.

Mara nyingi wahusika wakubwa-wakubwa hutumiwa na wasanii ili kusuta majivuno na maringo, pamoja na tabia za mabavu za baadhi ya watu katika jamii. Wahusika Zimwi na Joka katika majaribio waliyoyafanya E. Hussein na Penina Muhando wana uakilishi wa namna hiyo. Kwa hiyo basi hata ukubwa au udogo wa wahusika wa fasihi simulizi huweza kutumiwa katika kukosoa na kusahihisha mienendo ya baadhi ya wanajamii.

Hata hivyo haimaanishi kuwa wahusika wa aina hiyo hapo juu ndio tu walioko katika fasihi simulizi; kwani wako wahusika watu pia ambao hutumiwa kuwakilisha pande kuu mbili zinazovutana daima katika ulimwengu wa fasihi simulizi: upande wa wema au haki, na ule wa ubaya na dhuluma; ambapo wale wa upande wa wema na haki mara kwa mara huwashinda wahusika wabaya wenye dhuluma.

Kwa upande mwingine kunayo matumizi ya wahusika wasio miili, madubwana wa ajabu-ajabu, mashetani, na pia majini. Hawa hutumiwa kwa makusudi mbalimbali. Mara nyingi wanasaidia sana kujenga taharuki katika habari inayoelezwa. Tunapokutana na joka lenye vichwa sabini, halafu atokee kijana mdogo ajitape kuwa yeye ataliua, tunafuatilia kwa makini na mioyo ikitudunda, matendo ya mhusika huyu kuliko tungeelezwa tu kuwa kulikuwa na joka kubwa. Wahusika wa aina hii pia hutumiwa kuwajenga wahusika watu. Tunapomwona mhusika mtu akishuka hadi katika ulimwengu wa majini na kuongea na kupata ushauri wa Mfalme wa Majini, sisi hadhira humwona mhusika huyu, hasa kama ni kiongozi, kuwa bora na imara kuliko wengine. Ijapokuwa wahusika wa namna hii wanatumiwa katika fasihi simulizi, kuwapo kwao hakupunguzi kuaminika kwa yale yanayoelezwa. Kinyume chake, yale yaelezwayo yanaaminika na kuisisimua hadhira zaidi ya vile ambavyo yangekuwa iwapo yangeelezwa kwa kutumia wahusika watu tu.

Tuchunguzapo matumizi ya wahusika katika fasihi simulizi tutaona wazi kuwa hawa hutegemea maeneo ya kijiografia. Kwa mfano, mhusika Kanga mara nyingi atapatikana katika fasihi simulizi itokanayo na jamii zenye kulima mtama, wakati ambapo Nyani na Tumbili mara nyingi watatoka katika jamii za kilimo cha mahindi. Wahusika katika fasihi simulizi hutumiwa wakati mwingine kiishara. Simba, kwa mfano, huwakilisha ufalme na utawala; Jogoo ni mkuu wa familia, naye huashiria siku njema anapowika; Fisi huwakilisha matumizi ya nguvu, uchoyo na ulafi; Kondoo ni kiwakilisho cha upole na hata wakati mwingine upumbavu; Sungura mara nyingi huashiria ujanja, wakati ambapo Mzee Kobe ni kisima cha busara na hekima; Tausi anasimamia uzuri na maringo; Bundi mara nyingi ni ishara mbaya ya balaa na hata kifo; na Nzige huonyesha njaa, na hata uroho na ulafi.

Katika sehemu ifuatayo tutakitumia kipengele hiki cha wahusika wa kifasihi simulizi kuona ni kwa namna gani kimeathiri majaribio ya fasihi andishi ya Kiswahili.

### 3.9.1 Wahusika wa kifasihi simulizi katika fasihi andishi ya Kiswahili

Pamoja na wahusika hao wa kifasihi simulizi waliotumika katika *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* na *Lina Ubani*, wako pia wahusika wa kifasihi simulizi katika kazi nyinginezo za fasihi andishi ya Kiswahili. Mathalani, katika riwaya fupi ya Shaaban Robert ya *Adili na Nduguze*, Adili anachanganyikana na hata kuwasiliana na majini, na nduguze Adili wanageuzwa kuwa manyani. Unyama wa nduguze Adili wa kumtupa ndugu yao baharini ili tu wamrithi mpenzi wake na wairithi mali yake ni kielelezo tu cha unyama wa ubepari ambao ulikuwa umeshashamiri hata enzi za Shaaban Robert. Ni pale tu wanapobadilika na kujivua uhayawani ndipo wanapogeuzwa kuwa watu.

Mara kwa mara wahusika katika fasihi simulizi wanawakilisha pande kuu mbili: upande wa wema/haki na upande wa ubaya/uonevu.. Labda ni katika misingi hii ndimo ambamo hata baadhi ya waandishi wa fasihi ya Kiswahili wameathiriwa katika uundaji wao wa wahusika. Sifa na majina ya wahusika wao hubaki kuwa ileile tangu mwanzo hadi mwisho. Mfano mzuri wa waandishi wa namna hii ni ule wa E. Kezilahabi katika riwaya yake ya *Rosa Mistika* ambamo majina ya wahusika wake yanawakilisha tabia zao zisizobadilika tangu mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Tukitumia mifano ya Rosa Mistika, Flora, Regina na Emmanuel tunaweza kulithibitisha hili.

Rosa Mistika, pamoja na kuwa ni jina jingine la Bikira Maria, lakini linamaanisha ua waridi lenye fumbo. Kwa hiyo jina la mhusika huyu ni lile la ua moja tu. Flora maana yake ya asili ni mimea, kwa hiyo jina la mhusika huyu si la ua wala mmea mmoja tu bali linajumuisha *mimea yote*. Huenda mwandishi alitutaka tumwone Rosa kuwa yu dhaifu sana kama ua moja tu alinganishwapo na Flora ambaye anawakilisha mimea yote. Haya yanadhihirika hata katika maelezo tunayopewa, kuhusu wahusika hawa mwanzoni mwa riwaya hii (uk. 4):

> Rosa alikuwa msichana mzuri, mrefu kiasi, mnyenyekevu na mnyamavu. Kama akienda kuogakisimani utamwona kabla ya kuvua nguo anaanza kuangalia huku na huko, huvua, huoga upesiupesi, huvaa, huchukua maji na kurudi nyumbani. Alikuwa hapendi kuangaliwa kwa muda mrefu. Ukimwangalia machoni huinamisha kichwa.
>
> Flora akienda kuoga hujiangaliaangalia kwa muda mrefu kabla ya kuoga. Hutazama matiti yake ambayo sasa yalikuwa yanaanza kuwa makubwa; hujipapasapapasa kwa mikono kutoka mgongoni mpaka pale matako yanapotelemkia; halafu tena hujiangaliaangalia. Hata kama amemaliza kuoga, hungoja mpaka jua limkaushe ndipo avae. Akienda saa nane kisimani atarudi saa kumi na moja na jiwe lake mkononi, ingawa kisima kilikuwa maili moja tu kutoka nyumbani. Kila mara alitukanwa na mama yake kwamba alikuwa mvivu. Regina akisema kwenda kulima, yeye hubeba mtoto ubavuni. Akiambiwa kuweka moto jikoni, yeye huchukua majiani kutoka paa la jiko.

Maelezo haya ni ya makusudi kabisa yanayotutaka tuwaone wasichana hawa wawili kuwa ni tofauti. Mmoja ni dhaifu, na mwingine ni imara zaidi. Huenda ndiyo maana hadi mwishoni mwa riwaya hii, Flora anastahimili misukosuko ya maisha na anabaki kuwalea wadogo zake baada ya vifo vya wazazi na dada yao, wakati ambapo Rosa anashindwa kustahimili vishindo hivyo vya maisha na anajiua. Na hili linatufanya mwishoni mwa riwaya hii tukubaliane kwa kiasi kikubwa na Zakaria ambaye anakana kabisa na kusema kuwa si yeye aliyesababisha kujiua kwa Rosa anaposema, "Ee Mungu wangu. Haya yote yamctokea *kwa sababu ya ubaya na udhaifu wake (Rosa) mwenyewe.*" (uk. 98, msisitizo ni wangu). Hadhira inatakiwa iyapime yote haya sambamba na hulka ya Rosa, na inatakiwa imlinganishe Rosa na dadake mdogo, Flora, wote wamekulia na kupitia maisha karibu sawa – tangu ya malezi makali ya baba yao hadi ya shuleni, mbali na nyumbani na mbali na malezi makali ya mzee wao, ambako kuna kukutana na wavulana. Hasta hivyo, maisha hayo yanamshinda Rosa wakati ambapo Flora anayashinda. Mimea huweza kustahimili vishindo vya vurugu za hali ya hewa kuliko ua moja ambalo linanyauka na kudondoka kiurahisi.

Katika dini ya Kikristo, Emmanuel ni jina lingine la Yesu Kristo, nalo lina maana ya "Mungu yu pamoja nasi". Kuzaliwa kwa Emmanuel kunaleta uhusiano mzuri kidogo pamoja na amani katika familia ya Zakaria na Regina kwani huyu ni mtoto wa kiume ambaye Zakaria amekuwa akimlilia siku zote akimlaumu Regina kwa kumzalia wanawake tu kama iwelezwavyo ukurasa wa 23:

> Wale vijana walikimbia bila kuangalia nyuma. Walifikiri bado anawafuata. Zakaria aliwasikia kwa mbali wakimtukana.
>
> Mshenzi, utaoza na binti zako!"
>
> Zakaria hakuwajibu lolote. Regina na Rosa walikuwa wamenyamaza tu.
>
> "Mshenzi, unanizalia wasichana tu! Unaniletea taabu nyumbani bure tu!" Zakaria alifoka.
>
> Regina hakujibu; aliogopa kumdhihaki...

Kinyume na hali hiyo ya kukosekana kwa amani na furaha katika mji wa Zakaria, tukio la kuzaliwa kwa Emmanuel linaelezwa ifuatavyo:

> Zakaria alirudi usiku nyumbani siku hiyo. Alikuwa amekwishapata habari hizo njema njiani. Alimbeba mtoto. Alimpa pongezi mke wake.
>
> "Regina! Sasa mji huu umekuwa wako."...
>
> Usiku huo Zakaria aliimba aleluya karibu usiku kucha. Kesho yake alikwenda posta. Mke wake alishangaa kumwona jioni anarudi na vitu vyote alivyokuwa ametaja. Alianza kupata sauti. Alianza kuzungumza kwa furaha. Hata watu wa kijijini waliona ajabu... (kur. 24 – 25)

Emmanuel, basi, kama jina lake linavyomaanisha, analeta furaha kwa muda katika nyumba ya Zakaria na Regina.

Katika riwaya hii, Regina ni mhusika ambaye amependelewa kuliko wahusika wengine wote. Maana ya jina Regina ni malkia, na kwa hakika, ukiondoa umasikini wa vitu alio nao regina, mhusika huyu amepewa sifa za umalikiaumalkia. Tangu mwanzo hadi mwisho tunamwona mhusika huyu kuwa ni mama mwadilifu ambaye anawalea watoto wake kwa mapenzi makubwa sana. Ana huruma nyingi na pia hata anapoonewa na Zakaria ambaye kwa kiasi kikubwa ni mhusika hasi, mlevi, mwizi, na mgomvi; hatumwoni akilalamika sana. Zakaria anapoiba pesa za ada ya Rosa, Regina anajishughulisha kutafuta pesa zingine. Pamoja na matatizo mengi aliyopewa na Zakaria maishani mwake, bado tunamwona Regina akianguka na kufa mara tu anapomwona mumewe amekufa. Ndiyo maana hata katika makaburi matatu ya Rosa, Regina na Zakaria, ni juu ya kaburi la katikati la Regina ndiko ambako kumeota mchungwa wenye matunda mazuri sana kuliko michungwa ya makaburi ya Rosa na Zakaria. Mwandishi hapa ametumia ukatikati kama ishara itokanayo na dini ya Kikristo ambamo Yesu Kristo alisulubiwa katika msalaba ulio katikati ya ile ya wenye dhambi wawili. Ndiyo maana twaambiwa:

> Hata baada ya miaka kumi, matunda yalipokuwa yakiiva, watoto hawa walizoea kutoka Mwanza kuja kuchuma matunda kutoka ule mti wa katikati. Walikula **damu na mwili** wa mama yao. Walimkumbuka mama yao. (uk. 97; msisitizo ni wangu)

Sawa na Wakristo wanavyoamini kuwa Chakula cha Bwana au Sakramentiu Takatifu inayotolewa kwa mvinyo na mkate ni kiwakilisho cha mwili na damu ya Yesu, watoto hawa wanapokula machungwa mazuri yatokayo juu ya kaburi la mama yao huwa wanakula damu na mwili wa Regina. Kwa maana nyingine ni kwamba Regina anaendelea kuishi hata baada ya kufa.

Wahusika Rosa, Flora, Emmanuel na Regina tumewaita kuwa ni wahusika wa kifasihi simulizi kutokana na ukweli kuwa majina yao yanawakilisha matendo na nafasi zao katika hadithi hii; na kwa hakika, wahusika hawa wanabaki na sifa zao zilezile tangu mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Inaonyesha kuwa Kezilahabi alipoandika riwaya ya *Rosa Mistika* alinuia kwa makusudi kabisa kufanya majaribio ya kutumia uhusika wa kifasihi simulizi si katika maana ya majina ya wahusika wake tu, bali pia hata katika matendo na hulka zao ambazo zinabaki kuwa zilezile tangu mwanzo hadi mwisho kwani wabaya wanabaki kuwa wabaya na wema wanabaki kuwa wema.

### 3.10 Neno kuhusu fasihi ya majaribio

Itaonekana dhahiri kuwa katika makala hii istilahi ya *fasihi ya majaribio* imetumika bila kupewa maelezo kamili. Hili linatokana na ukweli kuwa si rahisi kueleza fasihi ya majaribio ni nini hasa. Inawezekana kabisa kuuliza, je kwa vile hakuna kazi moja ya fasihi inayofanana kabisa na kazi nyingine, si kila kazi mpya ya fasihi ina majaribio fulani?

Tunadhani kuwa ili kazi fulani iitwe kuwa ni fasihi ya majaribio haina budi kuambatana na upya ambao unaweza kueleweka kinadharia, na hata ikiwezekana nadharia hiyo iwe imeelezwa na mwandishi mwenyewe au na wahakiki wa wakati huo. Wakati ambapo E.Hussein na P. Muhando walianzisha mjadala kuhusu maana hasa ya tamthilia ya Kiswahili, wakaandikia suala hili tasnifu na makala mbalimbali ambazo zilihusu sanaa za maonyesho na fasihi simulizi ya Kiafrika, Kezilahabi alifanya majaribio na falsafa ya Udhanaishi, akionyesha kuwa maisha hayana maana kwani mtu anazaliwa ili afe. Kwa Kezilahabi, maisha ni fumbo sawa na Rosa alivyo ua waridi lenye fumbo. Nadharia hizi ndizo ambazo ziliwaongoza waandishi hawa hadi wakafanya majaribio ya kuzitumia kusana kazi zao.

Hii ina maana kwamba pamoja na majaribio madogomadogo ambayo yanajitikeza katika kila kazi mpya ya fasihi, ni yale tu ambayo yameambatanishwa na nadharia fulani na mijadala fulani ya kifasihi ndiyo tunayoweza kuyapa sifa za kuwa matapo fulani ya kimajaribio. Katika fasihi ya Kiswahili tunaweza kuyataja majaribio ya washairi huria, Kezilahabi, E. Hussein, M.M. Mulokozi, K.K. Kahigi, na wengineo wa aina hiyo, kuwa yaliunda tapo la majaribio katika ushairi wa Kiswahili. Hawa walikinzana na washairi wa kimapokeo waliosisitiza kuwa vina na mizani ni uti wa ushairi wa Kiswahili, wakatunga mashairi yasiyofuata arudhi na kanuni za urari wa vina na mizani. Haya yalikuwa ni majaribio yaliyoambatana na mjadala na malumbano makali.

Nionavyo mimi, majaribio hukoma kuitwa hivyo yanapotoa mazao ya kazi za kifasihi ambazo zinakubalika na hazionekani kuwa na upya tena. Leo hii tamthilia zinazotumia vipengele vya kifasihi simulizi na vya sanaa za maonyesho za Kiafrika si kazi za kifasihi zinazoonyesha upya wowote kwani zimezoeleka na kukubalika. Vivyo hivyo, mashairi yasiyofuata urari wa vina wala mizani hayaonekani mapya wala mageni kwani yameshazoeleka na yanasomwa shuleni na vyuoni. Kazi za namna hii basi, zimekoma kuwa za kimajaribio.

Upya wa nadharia pamoja na wa kazi za kifasihi zinazotokana na nadharia hizo ndio huunda majaribio. Huenda upya wa istilahi ya *Uhalisiamazingaombwe* ambayo leo hii inatumika kuzieleza zile kazi za kifasihi zinazounganisha uhalisi na uajabuajabu, unaunda kazi mpya za majaribio katika fasihi ya Kiswahili. Mathalani, upya huu unaonekana katika riwaya fupi za Kezilahabi za *Nagona* na *Mzingile*, na pia katika kazi mbalimbali za Said Ahmed Mohamed (Khamis) kama vile riwaya yake ya *Babu Alipofufuka* na hadithi fupi ya "Sadiki Ukipenda", ijapokuwa "upya" huu unaelekea kuwa wa kiistilahi zaidi ya kimtindo kwani, kama makala hii inavyoonyesha, vipengele vya maajabuajabu ndani ya fasihi ndivyo ambavyoi vimekuwa vikijenga msingi wa fasihi simulizi, hasa ndani ya ngano, visasili, visajanja, visapanda, vitendawili na tanzu zinginezo za fasihi hii ambazo zimekuwapo kwa karne nyingi. Kwa hakika, vipengele hivi pia vilishajaribiwa na kutumiwa na waandishi kama vile Shaaban Robert katika kazi zake za *Kusadikika*, *Kufikirika* na *Adili na Nduguze* kiasi kwamba

inakuwa vigumu kuona upya wa majaribio ya Kezilahabi, Mohamed na waandishi wengine wa kisasa wanaotumia mtindo wa Uhalisiamazingaombwe; mtindo ambao ni kama pombe ya zamani katika kibuyu kipya. Kama vile Mazrui na Mazrui (1995) wanavyodokeza kuwa mabadiliko ya lugha ni ushahidi wa mabadiliko mapana zaidi katika mfumo wa utamaduni unaohusika, inawezekana basi, kuwa hata mabadiliko ya fasihi nayo ni kielelezo cha mabadiliko mapana zaidi ya kitamaduni katika jamii husika. Swali la ni mabadiliko gani yanayozaa fasihi ya Kiswahili ya majaribio mahsusi katika wakati mahsusi na si wakati mwinginco, ni swali linalohitaji utafiti zaidi ili kujibiwa kwa usahihi zaidi.

## Marejeo


Hussein, E. 1976. *Jogoo Kijijini na Ngao za Jadi*. Nairobi: Oxford University Press.

Kezilahabi, E. 1975. *Rosa Mistika*. Dar es Salaam : Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. 1990, *Nagona*. Dar es Salaam: Dar-es-Salaam University Press.

Kezilahabi, E. *Mzingile*, 1992. Dar es Salaam : Dar es Salaam University Press.

Mazrui, A. na Mazrui, A. (1995). *Swahili, State and Society*. Nairobi. East African Educational Publishers.

Mohamed, S. A. 2001. *Babu Alipofufuka*. Nairobi : The Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, Said Ahmed, *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine*, Nairobi : The Jomo Kenyatta Foundation, 2002.

Muhando, P. *Lina Ubani*, 1982, Dar es Salaam : Dar es Salaam University Press.

Robert, Shaaban (1972) *Adili na Nduguze*, Nairobi : Nelson.